



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO



Unapojibu tafadhali taja;

Kumb. Na LA.152/215/01/27

Tarehe: 17 Aprili, 2025.

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
S.L.P 938,

DAR ES SALAAM.

Yah: **UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA VILLAGE CLIMATE
SOLUTIONS LIMITED (VCSL)**

Rejea somo tajwa hapo juu.

2. Naitambulisha kwako kampuni tajwa hapo juu, ambayo ina malengo ya kuwezesha vijiji mbalimbali hapa Tanzania kutekeleza biashara ya Kaboni kupitia mfumo unaojulikana kama "Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na ukataji miti hovy na uharibifu wa misitu" (MKUHUMI).
3. Mpango huu unasaidia utunzaji wa Misitu ya Asili inayomilikiwa na Vijiji, kwa mujibu wa Vifungu namba 4 (c) (i), 32 (1) (a) na (b) na 35 (6) (b) vya Sheria ya Misitu sura ya 323 ya Sheria za Tanzania.
4. VCSL inashirikiana na vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kutekeleza MKUHUMI, kwa lengo la kuzalisha na kuuza kredit za Kaboni, ambapo vijiji vitapata fedha zitakazosaidia maendeleo ya jamii hususani kuboresha kilimo, elimu ya sekondari na ufundi, afya, maji na upatikanaji wa hati miliki za ardhi.

Barabara ya Bigwa – Kisasi (Mvuha), S.L.P 1880, Morogoro, simu +255232613185

Nukushi: 0232613185, Barua Pepe: ded@morogorodc.go.tz, Tovuti:
www.morogorodc.go.tz


5. Mradi wa VCSL inajulikana kama *Village Climate Solutions Project (VCSP)* na umesajiliwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Mfumo wa Kimataifa wa Viwango vya Kaboni (*Verified Carbon Standards - VCS*) na Viwango vya Ubora (*Climate, Community and Biodiversity – CCB standards*) kupitia akaunti namba 1325.

6. Katika Wilaya ya Morogoro, Mradi huu unatekelezwa katika vijiji vifuatavyo (Ramani imeambatishwa)

- i) Mlilingwa
- ii) Diguzi
- iii) Matuli
- iv) Tununguo
- v) Lulongwe

7. Nawaomba Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kushirikiana na kampuni hii katika masuala yote yanayohusiana na uwekezaji na utekelezaji wa mradi huu ili kuhakikisha mafanikio yake na manufaa kwa jamii.

8. Natanguliza shukrani zetu kwa ushirikiano wako.


ALICE N. ERIYO

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MOROGORO

Barabara ya Bigwa – Kisasi (Mvuha), S.L.P 1880, Morogoro, simu +255232613185

Nukushi: 0232613185, Barua Pepe: ded@morogorodc.go.tz, Tovuti:
www.morogorodc.go.tz